

SHEREHE YA KUORODHESHA KWA HATIFUNGANI YA JAMII (SOCIAL BOND) YA NMB KWENYE SOKO LA HISI LA DAR ES SALAAM (DSE) - TAREHE 12 DESEMBA, 2023.

Toleo la Kwanza la Programu ya Hatifungani ya NMB ambalo limezinduliwa tarehe 12 Desemba 2023 lina thamani ya **shilingi bilioni 212** ambayo ni mafanikio ya **asilimia 284** toka kwa wawekezaji wapya (New Bondholders at the CSD) zaidi ya 4,900 na **Dola za Kimarekani milioni 73** ambayo ni mafanikio ya **asilimia 730** ikilinganishwa na **Dola za Kimarekani milioni 10** walizokuwa wakizitafuta mwanzoni.



Kuanzia Novemba 1999 DSE imenorodhesha jumla ya Hatifungani 27 (NMB Jamii Bond itakuwa ya 28) za Makampuni kutoka kwa makampuni 15. Nyingi ya Hatifungani hizo zimekwisha iva.

Kwa sasa DSE ina jumla ya **hatifungani 7** zitakazoiva kwa vipindi tofauti kati ya Juni 2024 na Oktoba 2028. Hatifungani ya Jamii ya NMB itakuwa ya **8** na **itaongeza thamani ya hatifungani za makampuni**

zilizopo Sokoni kwa zaidi ya asilimia 65 kutoka Shilingi 326 bilioni mpaka Shilingi 538 bilioni na pamoja na Dola za Kimarekani 73 milioni.

Kati ya April 2022 na Desemba 2023 DSE imeorodhesha hatifungani 5 ikiwa ni pamoja na hii ya NMB. Hii inathibitisha kuwa Soko letu linatekeleza kile kinachatajariwa katika kukuza uchumi.

